

**HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA**  
(Barua zote ziandikwekwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu: +255 27- 2641105

Fax: +255 27- 2641414

Barua pepe: [ded@muhezade.go.tz](mailto:ded@muhezade.go.tz)

Tovuti: <http://www.muhezade.go.tz> TANZANIA.



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W),  
S.L.P. 20  
MUHEZA – TANGA

Kumb.Na. HW/MUH/L.90/4 VOL III/125

03/03/2022

Afisa Mtendaji Kata  
Kata ya Mhamba  
S.L.P 20,  
MUHEZA.

**YAH: TAARIFA YA UKAGUZI WA ENEO LILILOPENDEKEZWA KUPEWA  
MWEKEZAJI KIJJI CHA BWITINI NA MTO WA MBUZI.**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Muheza kupitia wataalamu wake ilifanya ukaguzi tarehe 29/01/2022 kwenye eneo lililopendekezwa kupewa mwekezaji na kubaini kuwa eneo hilo lililopendekezwa lina ukubwa wa Ekari 991.4 sawa na Hekta 401.20.

Aidha, zoezi la ukaguzi lilizingatia maeneo yanayozunguka shamba yaani Hifadhi ya Msitu wa Kwani na Mamlaka ya Maji ya mto Pangani. Baada ya kuhakiki maeneo ya majirani tajwa hapo juu imebainika kuwa jumla ya Ekari 453.1 kati ya Ekari 991.4 ya eneo pendekewa zipo ndani ya mipaka ya Hifadhi ya msitu wa Kwani na jumla ya Ekari 538.3 zipo nje ya mipaka ya msitu wa kwani. Hivyo kutokana na utambuzi huo eneo lenye ukubwa wa Ekari 538.3 ndio lipo salama kwa uwekezaji (nakala ya ramani imeambatanishwa).

Hata hivyo, katika eneo la Ekari 538.3 kuna mabwawa matatu yanayotumiwa na wananchi kwa uvuvi ili kujipatia kipato na chakula, tunashauri pawepo na majadiliano na maridhiano kati ya mwekezaji na wananchi kabla ya utekelezaji wa mradi ili kuepusha migogoro.

Taratibu za upimaji na umilikishwaji zitafulwa baada ya maridhiano tajwa hapo juu.

ISSA S. MSUMARI  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
MUHEZA

Nakala. Mhe. Diwani Kata ya Mhamba  
Mkurugenzi kampuni ya Ragrisa RTS Kuku LTD

kwa taarifa  
kwa taarifa

KAMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
MUHEZA